FUNZO LA 41

1. Je, kwa nini Mungu hunena na watu mara kwa mara?
-Ili waokolewe.

2. Je, kwa nini Mungu alimtaka Yonah aende Ninawi?
-Kwa sababu Mungu aliwapenda watu wa Ninawi.
-Kwa sababu Mungu alitaka kuwaokoa watu wa Ninawi kutoka kwa nguvu za dhambi, kifo na Shetani.

3. Je, kwa nini Yonah alitoroka?
-Yonah alitoroka kwa sababu hakutaka kwenda kwa mji wa Ninawi.

4. Je, kwa nini Yonah hakutaka kwenda kwa mji wa Ninawi?
-Kwa sababu watu wa Ninawi walikuwa waovu sana.
-Kwa sababu watu wa Ninawi walikuwa adui wa Israeli.
-Kwa sababu Yonah hakutaka Mungu awaokoe watu wa Ninawi.

5. Je, Yonah aliweza kutoroka kutoka kwa Mungu?
-La.

6. Je, Yonah aliweza kujificha kutoka kwa Mungu?
-La.

7. Je, Yonah aliweza kuepuka Mungu?
-La.

8. Je, Mungu alifanya nini Yonah alipokataa kumtii kwa kukataa kwenda Ninawi?
-Mungu alituma samaki mkubwa akammeza Yonah.



9. Je, Yonah alikaa siku ngapi tumboni mwa samaki?
-Siku tatu mchana na usiku.

10. Je, Yonah aliweza kujiokoa kutoka tumboni mwa yule samaki mkubwa?
-La.

11. Je, ni nani aliyeweza kumuokoa Yonah?
-Mungu.

12. Je, watu wote wanafananaje na Yonah?
-Kama vile Yonah hakuweza kujiokoa katika tumbo la yule samaki mkubwa.
-Watu wote hawawezi kujiokoa kutoka kwa nguvu za dhambi kifo na Shetani.

13. Je, Mungu alifanya nini Yonah alipokubali kuwa hakumtii Mungu na alitenda dhambi dhidi ya Mungu?
-Mungu alimfanya yule samaki mkubwa kumtapika Yonah katika nchi kavu.

14. Je, baada ya Mungu kumuokoa Yonah, alimwambia kuwa si lazima aende Ninawi?
-La.

-Mungu habadiliki.
-Mungu kamwe habadiliki.

-Mungu bado alimtaka Yonah awapelekee watu wa Ninawi ujumbe wake.

15. Je, watu wa Ninawi walisikiliza ujumbe wa Mungu ambao Yonah aliwaambia?
-Ndiyo.

16. Je, watu ambao Mungu aliwachagua wawe wajumbe wake wa kuwaambia watu ujumbe wake, waliitwaje?
-Manabii.

17. Je, manabii waliwaambia nini watu?
-Waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

18. Je, nini kingewafanyikia makabila kumi ya Israeli iwapo hawangeacha njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu?
-Mungu angewatuma Waasiria wayashinde makabila kumi ya Israeli na kuwachukua kuwa watumwa wao.

19. Je, nini kingewafanyikia makabila mawili ya Yuda iwapo hawangeacha njia ya dhambi na kufuata njia ya Mungu?
-Mungu angewatuma Wababeli wayashinde makabila mawili ya Yuda na kuwachukua kuwa watumwa wao.

-Ingawaje miaka mingi ilipita tokea Mungu aahidi kumtuma Mwokozi, je, Mungu alisahau ahadi yake?
-La.

-Mungu aliwaahidi Adamu na Hawa kwamba atamtuma Mwokozi.



-Mungu aliwaahidi Ibrahamu, Isaka na Yakobo kwamba atamtuma Mwokozi.

-Mungu aliwaahidi Musa na Waisraeli kuwa atamtuma Mwokozi.

-Mungu aliwaahidi mfalme Daudi na mfalme Suleimani kwamba atamtuma Mwokozi.

-Mungu hakusahau ahadi yake ya kumtuma Mwokozi.

-Ingawaje Waisraeli hawakumwamini Mungu, je, Mungu aliamua kutokumtuma Mwokozi?
-La.

-Ingawaje Waisraeli hawakumwamini Mungu, je, mbona bado Mungu aliamua kumtuma Mwokozi?

-Kwa sababu Mungu anawapenda watu wote.

-Kwa sababu Mungu anataka kuwaokoa watu wote kutoka kwa nguvu za dhambi, kifo na Shetani.

-Kwa sababu Mungu hataki yeyote aende katika Ziwa la Moto wa Milele.

-Je, Mungu aliwapa nani Ujumbe wake kuhusu kuja kwa Mwokozi?

-Manabii.

-Je, ujumbe ambao Mungu aliwapa manabii kuhusu kuja kwa Mwokozi uliandikwa wapi?

-Katika kitabu cha Mungu, Biblia.

-Kabla ya Mungu kumtuma Mwokozi, Mungu alipanga kila kitu ambacho kingemfanyikia Mwokozi.

-Je, Mungu alisema nini kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 9:7a

7-Maongeo ya enzi yake na amani Hayatakuwa na mwisho kamwe, Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; Kuuthibitisha na kuutegemeza Kwa hukumu na kwa haki, Tangu sasa na hata milele.

-Mungu alisema kwamba Mwokozi atakuwa wa uzao wa Daudi na kuwa atakuwa mfalme milele.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 7:14

14-Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli.



-Mungu alisema kuwa Mwokozi hatakuwa na baba mwanadamu au mama mwanadamu ila atazaliwa na bikira.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Mika 5:2

2-“Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele.”

-Mungu alisema kwamba Mwokozi atazaliwa katika mji wa Bethlehemu.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Hosea 11:1

1-“Israeli alipokuwa mtoto, nalikuwa nikimpenda, nikamwita mwanangu atoke Misri.”

-Mungu alisema kuwa atamuita Mwokozi kutoka Misri.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 11:2

2-Na roho ya Bwana atakaa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya shauri na uweza, roho ya maarifa na ya kumcha Bwana;

-Mungu alisema kwamba Mwokozi ataongozwa na Mungu Roho Mtakatifu.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 53:4-5

4-Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; Lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa.
5-Bali alijeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake, Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atateseka kwa ajili ya watu wote.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 41:9

9-Msiri wangu tena niliyemtumaini, Aliyekula chakula changu, Ameniinulia kisigino chake.



-Mungu alisema kuwa Mwokozi atasalitiwa na rafiki.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zakaria 11:12-13

12-Nikawaambia, Mkiona vema, nipeni ujira wangu; kama sivyo, msinipe. Basi wakanipimia vipande thelathini vya fedha, kuwa ndiyo ujira wangu.
13- Kisha Bwana akaniambia, Mtupie mfinyanzi kima kizuri, hicho nilichotiwa kima na watu hao. Basi nikavitwaa vile vipande thelathini vya fedha, nikamtupia huyo mfinyanzi ndani ya nyumba ya Bwana.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atauzwa kwa vipande thelathini vya fedha.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 27:2

2-Watenda mabaya waliponikaribia, Wanile nyama yangu, Watesi wangu na adui zangu, Walijikwaa wakaanguka.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atashuhudiwa uongo.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 50:6

6-Naliwatolea wapigao mgongo wangu, na wang'oao ndevu mashavu yangu; sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atapigwa na kutemewa mate.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 53:7

7-Alionewa, lakini alinyenyekea, Wala hakufunua kinywa chake; Kama mwana-kondoo apelekwaye machinjoni, Na kama vile kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake; Naam, hakufunua kinywa chake.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi hatasema lolote atakapo shutumiwa.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 53:3

3-Alidharauliwa na kukataliwa na watu; Mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko; Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu.



-Mungu alisema kuwa watu watamkataa Mwokozi.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 69:4

4-Wanaonichukia bure ni wengi Kuliko nywele za kichwa changu. Watakao kunikatilia mbali wamekuwa hodari, Adui zangu kwa sababu isiyo kweli. Hata mimi nalilipishwa kwa nguvu vitu nisivyovichukua.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atachukiwa bila sababu.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 22:16

16-Kwa maana mbwa wamenizunguka; Kusanyiko la waovu wamenisonga; Wamenizua mikono na miguu.

-Mungu alisema kuwa miguu na mikono ya Mwokozi itatobolewa.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 22:18

18-Wanagawanya nguo zangu, Na vazi langu wanalipigia kura.

-Mungu alisema kuwa mavazi ya Mwokozi yatapigiwa kura.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 22:6-7

6-Lakini mimi ni mdudu wala si mtu, Laumu ya wanadamu na mzaha wa watu.
7-Wote wanionao hunicheka sana, Hunifyonya, wakitikisa vichwa vyao;

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atafanyiwa mzaha na kutusiwa.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 53:12

12-Kwa hiyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, Naye atagawanya nyara pamoja nao walio hodari; Kwa sababu alimwaga nafsi yake hata kufa, Akahesabiwa pamoja na hao wakosao. Walakini alichukua dhambi za watu wengi, Na kuwaombea wakosaji.



-Mungu alisema kuwa Mwokozi atakufa pamoja na watu waovu.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Isaya 53:9

9-Wakamfanyia kaburi pamoja na wabaya; Na pamoja na matajiri katika kufa kwake; Ingawa hakutenda jeuri, Wala hapakuwa na hila kinywani mwake.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atazikwa na tajiri.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 16:10

10-Maana hutakuachia kuzimu nafsi yangu, Wala hutamtoa mtakatifu wako aone uharibifu.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atafufuka kutoka katika wafu.

-Je, Mungu alisema nini tena kumhusu Mwokozi ambaye angemtuma?

Tusome Zaburi 68:18

18-Wewe umepaa juu, umeteka mateka, Umepewa

vipawa katikati ya wanadamu; Naam, hata na wakaidi, Bwana Mungu akae nao.

-Mungu alisema kuwa Mwokozi atarudi Mbinguni.

-Kabla ya kumtuma Mwokozi, Mungu alipanga kila kitu ambacho kingemfanyikia Mwokozi.

-Manabii wa Mungu waliwaambia Waisraeli kumhusu Mwokozi ambaye Mungu angemtuma.

-Manabii wa Mungu pia waliwaambia Waisraeli waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Je, Waisraeli wengi waliwasikiliza manabii wa Mungu?
-La.

-Je, Waisraeli waliwafanyia nini manabii wa Mungu?

-Waliwaua.

-Je, kwa nini Waisraeli waliwaua manabii wa Mungu?

-Kwa sababu manabii waliwaambia Waisraeli waache njia ya dhambi na wafuate njia ya Mungu.

-Kwa sababu manabii waliwaambia Waisraeli kuwa Mungu ataadhibu dhambi yao kwa kifo.



-Kwa sababu Waisraeli walipenda dhambi yao na hawakutaka kumtii Mungu.

-Badala ya kuwasikiliza manabii, je, Waisraeli walisikiliza nani?

-Manabii wa uongo.

-Manabii wa uongo walisema kuwa walikuwa manabii wa Mungu, ila walikuwa manabii wa Shetani.

-Manabii wa uongo walikuwa wakisema kuwa Mungu hangeadhibu dhambi yao kwa kifo.

-Manabii wa uongo walikuwa wakisema kuwa walinena ukweli wa Mungu, lakini walinena nini?

-Uongo wa Shetani.

-Je, ni nani aliyenena kupitia kwa manabii wa uongo?
-Shetani.

-Hata leo, Shetani bado ananena uongo wake kupitia kwa watu?

-Ndiyo.

-Shetani husema kupitia kwa watu kuwa wasimfuate Mungu.

-Shetani husema kupitia kwa watu kuwa wafuate njia za mababu.

-Shetani husema kupitia kwa watu wasisikilize Neno la Mungu.

-Shetani husema kupitia kwa watu kuwa Neno la Mungu si kweli.

-Shetani husema kupitia kwa watu kuwa Mungu hataadhibu dhambi.

-Ijapokuwa Waisraeli waliabudu mifano walioifanya, je, walimwabudu Mungu katika hekalu?

-Ndiyo.

-Je, Mungu alikubali ibada ya Waisraeli walioabudu mifano walioifanya na pia kumwabudu Mungu katika hekalu?

-La.

-Je, kwa nini Mungu alikataa ibada ya Waisraeli walioabudu mifano walioifanya na kumwabudu Mungu pia hekaluni?

-Kwa sababu Mungu alijua kuwa walikuwa wakimwabudu kwa vinywa tu.

-Kwa kuwa Mungu alijua kuwa waliabudu mifano kwa mioyo yao.

-Je, ni nani ajuaye kila kitu mioyoni mwetu?
-Mungu.



-Mungu anaweza kuona ndani ya mioyo yetu.

-Mungu anajua iwapo tunamwabudu kwa vinywa tu ama kwa moyo.

-Je, Mungu anasema nini kuhusu mioyo yetu yote?

-Mungu anasema kuwa mioyo yetu yote imejaa dhambi.

-Ingawaje wengi wa Waisraeli waliabudu mifano, je, kuna baadhi yao ambao walimwabudu Mungu?

-Ndiyo.

-Kulikuwepo na wachache.

-Je, hao Waisraeli waliomwabudu Mungu walimsubiri nani?

-Walisubiri Mungu amtume Mwokozi.